

**HOTUBA YA MHESHIMIWA KAPT (MST) GEORGE H. MKUCHIKA
(MB), WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA WAKATI UZINDUZI
WA BODI YA USHAURI YA WAKALA YA NDEGE ZA SERIKALI
(TGFA),**

TAREHE 19 MEI, 2020 IKULU CHAMWINO, DODOMA

**Mheshimiwa *Baloz* *Mhandisi* John W. H. Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi na
Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala ya Ndege za Serikali;**

***Dkt.* Moses M. Kusiluka, Katibu Mkuu Ikulu;**

Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala ya Ndege za Serikali;

***Dkt.* Benjamin Ndimila, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Ndege za
Serikali;**

Watumishi wa Wakala ya Ndege za Serikali;

Mabibi na Mabwana.

Habari za asubuhi.

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema sisi sote. Pili napenda kutumia nafasi hii kumshukuru **Mheshimiwa *Dkt.* John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukuteua wewe ***Baloz* *Mhandisi* John W.H. Kijazi** ambaye pia ni Katibu Mkuu Kiongozi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala ya Ndege za Serikali (*TGFA*). Hii inaonyesha jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais amelipa uzito jukumu la Usimamizi wa *TGFA*. Napenda kukupongeza sana wewe pamoja na Wajumbe wa Bodi kwa uteuzi wenu.

Bodi hii imesheheni watu wenye nafasi kubwa Serikalini na kwenye taasisi za Umma. Kila mjumbe wa Bodi hii ni mtu mwenye weledi mkubwa katika eneo lake la kazi na taaluma. Hivyo, ni matarajio yangu kwamba mtatekeleza majukumu yenu kwa

ufanisi mkubwa ili kuiwezesha Serikali kutimiza azma yake ya kuimarisha usafiri wa anga nchini.

Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe, Wakala ya Ndege za Serikali ilianzishwa rasmi tarehe 17 Mei, 2002 kupitia Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997 kama ilivyorekebisha Mwaka 2009. Wakati wa kuanzishwa kwake, Wakala hii ilikuwa chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Tarehe 23 Aprili, 2018, Serikali iliamua kuihamisha Wakala hii kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwenda Ofisi ya Rais, Ikulu kwa Tangazo la Serikali Na. 252 la tarehe 8 Juni, 2018.

Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi, Wakala ya Ndege za Serikali inatekeleza majukumu makubwa matatu (3). Kwanza, ni kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa usalama na viwango vya hali ya juu. Pili, ni kuratibu na kusimamia ununuzi na ukodishaji wa ndege za Serikali kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*). Tatu, ni kuendesha na kufanya matengenezo ya ndege za Serikali kwa ufanisi unaozingatia viwango vya hali ya juu vya usalama.

Majukumu haya ni nyeti sana, ni matarajio yangu kwamba mtailinda imani na heshima kubwa aliyowapeni Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha kwamba mnaisimamia vizuri Wakala ya Ndege za Serikali ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe, kuimarisha usafiri wa anga ni moja ya vipaumbele vikubwa vya Serikali ya Awamu ya Tano. Sote tunafahamu kwamba hadi sasa Serikali imenunua ndege mpya 11. Kati ya ndege hizo, ndege nane (8) tayari zimeshapokelewa na zimeshakodishwa ATCL. Na kama alivyoeleza Mwenyekiti, ndege tatu (3) ndio zinatengenezwa na zinatarajiwa kuwasili nchini kati ya sasa na mwezi Juni, 2021. Lengo la Serikali ni kuona kwamba Tanzania inakuwa na Shirika la Ndege imara litakaloweza kushindana na mashirika mengine ya kikanda na kimataifa kwa kuanzisha na kuendesha safari nyingi za ndani ya nchi, za kikanda na za kimataifa.

Ngingependa nisistize pia kwamba suala la kuimarisha usafiri wa anga kwa kulifufua Shirika la Ndege la Tanzania ni moja ya ahadi za Chama cha Mapinduzi

iliyopo kwenye Ilani yake ya Uchaguzi ya Mwaka 2015. Hivyo, mageuzi makubwa yaliyofanyika kataika sekta ya usafiri wa anga katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano ni utekelezaji wa Ilani hii ya CCM.

Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe, mbali na ndege nane (8) zilizokodishwa ATCL, Wakala pia ina ndege nyingine nne (4) ambazo zinatumiwa kuwahudumia Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Ni jukumu lenu pia kuhakikaisha kwamba wakati wote ndege hizi zinasimamiwa vizuri na matengenezo yake yanafanyika kwa wakati na kwa ukamilifu ili kuweza kumpatia Mheshimiwa Rais pamoja na Viongozi Wakuu wa Kitaifa huduma bora na salama ya usafiri wa anga ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao.

Halikadhalika, simamieni kikamilifu taratibu za manunuzi ili kuweza kupata vifaa na huduma zinazoendana na thamani ya fedha.

Mmenieleza changamoto ya malipo ya fedha za mikataba ya ukodishaji wa ndege kwa ATCL. Kama Mwenyekiti ulivyowaelekeza Makatibu Wakuu, nitakaa na Waziri mwenzangu ili kuona namna ya kutatua tatizo hili. Katika suala hili, maelekezo ya Mheshimiwa Rais yako wazi, kwamba ATCL wahakikshe kwamba wanailipa Serikali kwa mujibu wa Mkataba wa Ukodishaji wa Ndege ili kuiwezesha Serikali kutoa huduma kwa wananchi.

Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe, suala lingine muhimu sana linalohitaji usimamizi wa karibu na makini ni kuhakikisha kwamba TGFA inakuwa na rasilimaliwatu yenye weledi na ya kutosha ili kukidhi matakwa ya kisasa katika umiliki na uendeshaji wa ndege.

Kama Mwenyekiti ulivyoieleza, kwa sasa nchini tuna uhaba wa wahandisi wa ndege wenye vyeti vinavyotambulika kimataifa. Litafutieni ufumbuzi suala hili, maana sasa tunazo ndege za kisasa tofauti na kipindi cha nyuma ambapo tulikuwa hatuna ndege – na pengine watu wengi hawakuona sababu ya kusomea taaluma za masuala ya ndege. Vilevile, hakikisheni kwamba mnaimarisha taaluma nyingine ambazo ni muhimu katika tasnia ya usafiri wa anga.

Ninafahamu kwamba katika mikataba ya ununuzi wa ndege mpya kuna fursa za mafunzo kwa ajili ya wataalam wetu. Hakikisheni mnatumia fursa hizo kwa ajili ya kuwapatia mafunzo watumishi wa Wakala katika maeneo yenye uhaba wa wataalam. Ni jukumu lenu kuhakikisha kwamba mnajenga uwezo wa ndani ili shughuli nyingi za matengenezo na ukaguzi wa ndege zetu zifanyike hapa hapa nchini na kwa kiasi kikubwa zifanywe na wataalam wazalendo.

Jambo hili ni muhimu kwa usalama wa Viongozi wetu na katika kupunguza gharama za matengenezo ya ndege zetu.

Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi, TGFA na ATCL zote ni taasisi za Serikali. Ni matarajio ya Serikali kuona taasisi hizi zinafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu. Bahati nzuri Mwenyekiti wa Bodi hii pia ndiye Mkuu wa Utumishi wa Umma nchini. Unayo mamlaka makubwa pamoja na rasilimali za kutosha unazoweza kuzitumia kuhakikisha kwamba taasisi hizi mbili zinafanya kazi kwa ushirikiano wenye tija. Tunatarajia pia kuona kwamba taasisi hizi zinabadilishana wataalamu ili kujengeana uwezo na kubadilishana uzoefu.

Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi, kimuundo, Bodi hii ni chombo cha kumshauri Waziri. Ni matarajio yangu kwamba mara kwa mara nitapatiwa ushauri wa namna ya kuboresha ufanisi wa Wakala ya Ndege za Serikali ili kuweza kufikia malengo ya Serikali. Kwa kumalizia, nisisitize kwamba ni matarajio yangu kwamba Bodi hii itasimamia kikamilifu Wakala ya Ndege za Serikali na kuhakikisha kwamba inakuwa na mipango na mikakati mizuri itakayoleta tija katika utekelezaji wa majukumu tuliyoikabidhi. Hili liende sambamba na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma na usimamizi wa makusanyo ya fedha ya Serikali yatokanayo na ukodishwaji wa ndege kwa ATCL.

Baada ya kusema hayo, sasa ninatamka kwamba **Bodi ya Ushauri ya Wakala ya Ndege za Serikali nimeizindua rasmi leo tarehe 19 Mei, 2020.**

Asanteni kwa kunisikiliza.